

Tafakuri ya Upolisemia na Usitari wa Ungonoshaji wa Maneno katika Kiswahili cha Mazungumzo

Mohamedi A. Ngunguti na Gastor C. Mapunda
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ikisiri

Kumeibuka tabia ya baadhi ya wawasiliani wa Kiswahili kuyapa tafsiri za kingono maneno ambayo hayahusiani moja kwa moja na ngono. Katika miktadha mingi ya kimawasiliano ni jambo la kawaida kwa baadhi ya wawasiliani kukihusisha na ngono chochote kismwacho; iwe kwa misingi ya viungo vya ngono, mitindo ya ngono, au tendo la ngono. Hali hiyo ndiyo ambayo katika makala hii tunaiita ungonoshaji. Licha ya kuwapo kwa viashiria vya kusambaa kwa ungonoshaji, nafasi yake kiisimu bado haijafahamika. Hilo ndilo lililoibua haja ya kufanya utafiti huu kwenye Kiswahili cha mazungumzo, huku tukijiuliza iwapo ungonoshaji unahusiana na polisemia au sitiari. Chanzo cha data za makala hii ni maktabani ambapo data zilikusanywa kwa mbinu ya uchanganuzi wa nyaraka. Data hizo zilizohusisha kauli mbalimbali zenye viashiria vya ungonoshaji zilizosemwa na watu mbalimbali na kunukuliwa na kuhifadhiwa katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii katika mfumo wa sauti au video. Mitandao ya kijamii tuliyoiteua na kuitumia ilikuwa *Youtube*, *Instagram* na *Facebook*. Makala hii basi imebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa, ungonoshaji wa maneno katika Kiswahili cha mazungumzo kwa kiasi kikubwa una sitiari ingawa polisemia pia hujitokeza.

Maneno Muhimu: *ungonoshaji, mazungumzo, wawasiliani, polisemia, na sitiari.*

Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Ingawa inafahamika kuwa dhima kuu ya lugha ni mawasiliano, ni jambo gumu kufafanua jinsi mawasiliano hayo yanavyofanywa kupitia lugha. Aghalabu, maneno hufungamanishwa na maana fulani au seti ya maana kadhaa kuwa ndiyo hasa maana ya neno fulani. Hata hivyo, watumiaji wa lugha hupigania uhuru wa kuyatumia maneno watakavyo na kuyapa tafsiri wazitakazo kwa kutumaini kwamba muktadha utawasaidia kuelewana. Ungonoshaji wa maneno ya Kiswahili katika mazungumzo ni mfano mmoja unaoweza kutolewa kushadidia hoja hiyo ambapo kumekuwa na tabia ya baadhi ya wawasiliani wa lugha ya Kiswahili kuyabebesha maana au tafsiri za kingono maneno ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja na ngono (taz. Reuster-Jahn na Kieβling, 2006; Elias 2016).

Kimuundo, makala hii ina jumla ya sehemu tano ambazo ni utangulizi na mapitio ya maandishi; nadharia na methodolojia; tafiti tangulizi; tafakuri ya upolisemia na usitari wa ungonoshaji wa maneno katika Kiswahili cha mazungumzo; na hitimisho.

Nadharia na Methodolojia

Katika sehemu hii, kama kichwa cha habari kinavyodokeza, tunajadili vipengele vya kinadharia tulivyovitumia ili kutuongoza katika kuchambua na kufafanua data na kufikia mahitimisho, pamoja na methodolojia, kwa maana ya mbinu zilizotumika kukusanya na kuchanganua data.

Nadharia

Kwa kawaida, ufafanuzi wa masuala ya kiutafiti huegemezwa katika nadharia fulani ili kuimarisha uhalali wake na kurahisisha uelewekaji wake. Ili kukidhi hitaji hilo, makala hii inaongozwa na Nadharia ya Semantiki Tambuzi ya Rosch (1978) na Nadharia Tambuzi ya Sitiari ya Lakoff na Johnson (1980). Nadharia ya Semantiki Tambuzi inajishughulisha na semantiki leksika ambapo semantiki hutazamwa kwa mitazamo mikuu miwili: kama 'ujenzi wa maana' na kama 'uwakilishi wa maarifa'. Nadharia hii imejengwa kwenye hoja kwamba maana ya leksimu ni udhanaishaji. Nadharia

hii inasema, “Maana ya leksimu si urejeleo wake kwenye kitu; wala uhusiano wake na ‘ulimwengu halisi’ ambao leksimu hiyo inaurejelea; bali katika dhana ya akilini kulingana na tajiriba aliyonayo mtu kuhusiana na kitu hicho au uhusiano huo”. Hii ina maana kuwa semantiki si thabiti na kwamba maarifa ya kisemantiki hayatenganishiki na maarifa ya masuala mengine ambayo si semantiki. Kimsingi, dhana ya Semantiki Tambuzi inayotungoza katika makala hii ni “ujenzi wa maana” ambapo inaelezwa kwamba maneno hayana maana iliyo tayari kutumiwa bali maana zake hujengwa na kuafikiwa ‘mkondoni’ kwa kutumia ‘mali ghafi’ za kimuktadha (Croft na Cruse, 2004; Cruse, 2011). Aidha, Mtazamo wa Sitiari kama Nyenzo ya Utambuzi ambao uliasisiwa na Lakoff na Johnson (1980) umetumiwa katika makala hii, hususani katika kipengele cha uchanganuzi wa data ambazo zilikusanywa. Mtazamo huu umejikita katika hoja kwamba sitiari si pambo tu la lugha bali ni sehemu ya mfumo wa utambuzi wa binadamu.

Methodolojia

Data zilizotumiwa kwenye makala hii zilikusanywa jijini Dar es Salaam nchini Tanzania ambapo mbinu ya uchanganuzi wa nyaraka ilitumika. Mbinu hii ilitumiwa kukusanya kauli zilizowahi kusemwa na watu mbalimbali ambazo zinafumbata ungonoshaji na ambazo zimepakiwa na kuhifadhiwa katika mitandao mbalimbali ya kijamii. Ingawa kuna mitandao mingi ya kijamii, data za makala hii zilikusanywa kutoka katika mitandao mitatu tu ya *YouTube*, *Instagram* na *Facebook*. Mitandao hii mitatu ilitolewa kwa sababu ilikidhi kigezo tulichojiweka cha kutumia mitandao ile tu ambayo kauli moja yenye viashiria vya ungonoshaji itapatikana katika mitandao miwili hadi mitano ikiwa imepakiwa na kuchangiwa au kutolewa maoni na wachangiaji. Katika mitandao hiyo mitatu, video zilezile zilipatikana kote. Hivyo, tulipitia mitandao hiyo mitatu tukakusanya jumla ya vipande kumi vya video na kusoma maoni yaliyotolewa na wachangiaji kuhusu video hizo. Maoni hayo ya wachangiaji yalitusaidia kubaini kwamba hata wachangiaji hao wamengonosha. Ili kuepuka makala hii kuwa ndefu kupita kiasi, tumefanya unukuzi na uchambuzi wa vipande sita tu vya video kati ya vipande kumi. Data zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli ambapo maelezo yametolewa katika kutafsiri na kufafanua data.

Tafiti Tangulizi Zihusianazo na Makala Hii

Katika sehemu hii tunaangalia tafiti na maandiko mbalimbali yaliyotolewa awali, hususani yale ambayo yanahusiana na maudhui ya makala hii. Tumezigawa tafiti hizo katika sehemu ndogondogo tatu kulingana na maudhui yake. Sehemu hizo ni ungonoshaji wa lugha, polisemia, na sitiari.

Ungonoshaji wa Lugha

Kadiri ya uelewa wetu, ungonoshaji wa lugha kama kipengele cha kiisimu haujawashughulisha watafiti wengi. Hata wachache ambao kazi zao zinaweza kuhusishwa na ungonoshaji hawakutumia istilahi ‘ungonoshaji’. Kazi za wataalamu hao ziliandikwa kwa mikabala ya lugha na jinsia, Kiswahili cha mtaani, mabadiliko ya maana, na upanuzi wa maana. Baadhi ya wataalamu hao ni Eckert na Connell-Ginet (2003), Reuster-Jahn na Kießling (2006), Kibiki (2012) na Elias (2016). Kwa mfano, wakimnukuu Baker (1975), Eckert na McConnell-Ginet (2003) wanaeleza jinsi wazungumzaji wa lugha ya Kiingereza wanavyoyatumia kisitiari maneno kama: *score* (funga goli), *screw* (funga/toboa kwa sukulubu), *lay* (laza), *bang* (bamiza) na *hump* (nundu) kurejelea ngono. Wataalamu hawa wanaendelea kufafanua kwamba, maneno haya yatumikapo kisitiari kurejelea ngono, aghalabu huwasawiri wanaume kama watenda na wanawake kama watendwa katika tendo la ngono. Wakilitolea mfano neno *screw*, waandishi hawa wanamnukuu Ross (1981) anayesema kwamba neno *srew* huashiria hali ya nguvu na uharibifu ambapo mtenda (mwanamume) husawiriwa kama mtu atumiaye nguvu kubwa tendoni ambapo husababisha maumivu na/au uharibifu kwa mtendwa (mwanamke) mithili ya nguvu itumikayo wakati wa kupenyeza sukulubu kwenye ubao na maumivu ‘yaupatao’ ubao huo.

Nao Reuster-Jahn na Kießling (2006:27) wanaieleza ‘ngono’ kuwa mojawapo ya nyanja za kimaana katika Kiswahili cha mtaani. Wanasema: “Uwanja huu wa ngono hutawaliwa na maneno

yanayorejelea tendo la ngono. Maneno yanayojitokeza katika uwanja huu kwa kiasi kikubwa huwakilisha mtazamo wa kiume ambapo ‘sitiari ya chakula’ hujitokeza sana.” Wataalamu hawa wanaeleza zaidi kwamba kuna msisitizo mkubwa wa dhima ya utenda kwa wanaume katika Kiswahili cha mtaani inayoelezwa kwa kutumia vitenzi kama piga, chapa, gonga, kaza na tia. Vitenzi hivi huakisi aina fulani ya nguvu na ubabe wa wanaume dhidi ya wanawake katika tendo la ngono. Hata hivyo, wataalamu tuliwarejelea hawakuwa na madhumuni ya kueleza ungonoshaji katika lugha ya Kiswahili unahusiana na kipi hasa kati ya polisemia na sitiari. Lengo la makala hii ni kutafakari upolisemia na usitiari wa ungonoshaji wa maneno ya Kiswahili cha mazungumzo ili kubaini upande ambako ungonoshaji huegemea.

Tafiti nyingine ni za Kibiki (2012) na Elias (2016). Wakati utafiti wa Kibiki unahusu mabadiliko ya maana katika vitenzi vya Kiswahili, utafiti wa Elias unahusu upanuzi wa maana katika mazungumzo ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti wa Kibiki (2012) yanaonesha kwamba maana hubadilika kutegemea nomino vinazoambatana na vitenzi, wakati matokeo ya utafiti wa Elias (2016) ni kwamba kuna ongezeko kubwa la maana za kingono katika mazungumzo ya Kiswahili. Makala hii inajaribu kutafakari dhima ya ungonoshaji huo ambapo inahoji iwapo ungonoshaji wa maneno ya Kiswahili katika mazungumzo ni polisemia au sitiari.

Mabadiliko ya Maana katika Kiswahili

Katika sehemu hii, mabadiliko ya maana yametazamwa kwa namna mbili: mabadiliko kipolisemia na mabadiliko kisitiari. Tukianza na namna ya kwanza ya mabadiliko, Mwendamseke, (2016) anajadili uelekeo wa mabadiliko ya maana katika polisemia katika Kiswahili huku akichunguza jinsi maana za kipolisemia zilivyowasilishwa katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* ya TUKI (2013). Hoja kuu inayoibuliwa na Mwendamseke ni kwamba, maana za kipolisemia hazitokei ghafla kama ajali. Hii ina maana kwamba polisemia ni matokeo ya mabadiliko ya maana hususani upanuzi wa maana na hivyo mabadiliko ya maana ni sababu kuu ya kuwapo kwa maana za kipolisemia katika Kiswahili.

Kwa upande wa mabadiliko ya maana kisitiari katika Kiswahili, tutaangalia kwa muhtasari tafiti zilizofanywa na watafiti wawili ambao ni Asheli (2011) na Makame (2015). Kwa kuanza na Asheli (2011), yeye alichunguza ufanisi wa kimawasiliano wa sitiari kwenye vichwa vya habari vya magazeti matatu ya Kiswahili nchini Tanzania. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba sitiari zina dhima ya upanuzi wa maana, ambapo, kwa mujibu wa wanasemantiki (taz. Ullmann 1962) na wanaisimu-historia na isimu-linganishi (taz. Campbell 2004), sitiari ni moja ya aina za mabadiliko ya maana.

Naye Makame, (2015) alichunguza jinsi maana za kisitiari zinavyojitokeza katika nomino za Kiswahili. Matokeo yanaonesha kwamba, nomino za Kiswahili hupokea maana za kisitiari baada ya wazungumzaji kuhamisha sifa au dhana fulani kutoka katika kitu kimoja na kuipeleka katika kitu kingine. Hali hiyo husababisha neno kupokea maana ya ziada ambayo ni maana ya kisitiari.

Dhana na Sifa za Polisemia

Polisemia ni hali ambapo neno moja hutokea kuwa na seti ya maana tofauti (Palmer, 1976). Aidha, Leech (1981) anafasili polisemia kuwa hali ya umbo moja la kiisimu (yaani neno) kuwa na maana zaidi ya moja. Akizungumzia dhana ya polisemia, Cruse (1986:80) anasema; “Ni jambo la kawaida kulielezea neno lenye maana kadhaa kuwa lina sifa ya polisemia...” Fasili hizi hazituwezeshi kutofautisha polisemia na homonimia kwa vile sifa zilizoenezwa kupitia fasili hizi hujitokeza katika dhana zote mbili zilizoongelewa, yaani polisemia na homonimia.

Kwa upande mwingine, TUKI, (2014) wanafasili polisemia kuwa ni neno lenye maana mbili au zaidi zinazokaribiana. Licha ya TUKI kukanganya dhana (polisemia) na neno (polisemi), fasili hii ni angavu zaidi kwani inatusaidia kutofautisha polisemia na homonimia. Maelezo kama haya yanatolewa pia na Saeed, (2004) ambaye anaeleza kwamba kuna njia ya asili inayotumiwa katika taaluma ya leksikolojia kutofautisha homonimia na polisemia. Anaeleza zaidi kwamba dhana zote mbili zinahusu maana nyingi za neno moja la kifonolojia, lakini polisemia hujitokeza pale ambapo fahiwa hizo za neno moja huonekana kuwa na uhusiano. Naye Cruse, (2006) anaonesha mtazamo kama huu kuhusu

polisemia kwa kueleza kwamba, inapotokea kwamba kuna uhusiano wa kimaana kati ya fahiwa kadhaa za neno basi tunasema kwamba neno hilo ni la kipolisemia. Kwa maneno mengine ni kwamba, Cruse, (keshatajwa) anautazama upolisemia kama hali ya neno kuwa na maana kadhaa zinazohusiana.

Kwa kuzingatia maelezo yaliyotolewa na wataalamu waliorejelewa hapo juu, (kama Palmer, 1976; Leech, 1981; Cruse, 1986; TUKI, 1990 na 2014; Saeed, 2004; Cruse, 2006 na 2011) na wengineo, tunaweza kudondoa sifa kadhaa za polisemia. Sifa hizi ndizo tutakazozitumia katika tafakuri ya ungonoshaji wa Kiswahili cha mazungumzo iwapo ni polisemia au la.

Mosi, polisemia ni hali ya neno kuwa na maana zaidi ya moja ambapo neno lenyewe huitwa polisemi, na kwamba maana za kipolisemia hukaribiana kwani huchanua kutoka kwenye maana msingi moja. Katika tafakuri yetu ya polisemia katika ungonoshaji, tutaangalia ikiwa maneno ngonoshi huwa na maana zaidi ya moja zinakaribiana. Pili, polisemia ni hali ambayo hujitokeza taratibu katika lugha kwani ni matokeo ya mabadiliko ya maana. Katika hili, tutatafakuri iwapo kuna dalili za aina yoyote ya mabadiliko ya maana katika ungonoshaji ambazo ni za kipolisemia. Na sifa ya tatu ni kwamba, polisemia ni moja ya vyanzo vya utata wa maana katika lugha na katika mawasiliano. Katika kutafakuri polisemia katika ungonshaji, tutazinagatia pia sifa hii ambapo tutajiuliza iwapo kuna utata wa maana katika ungonoshaji, utata ambao unatokana na maneno ngonoshi tunayoweza kusema kwamba ni polisemi.

Dhana, Mitazamo na Sifa za Sitiari

Dhana ya sitiari imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali kwa namna tofauti lakini zinazoshabihiana. Kwa mfano, TUKI (1990) wanaeleza kwamba sitiari ni mtindo wa usemaji ambao hulinganisha vitu au watu bila kutumia viunganishi. Naye Massamba (2004) anaeleza kwamba sitiari ni namna ya usemaji ambapo kitu hupewa jina la kitu kingine kwa namna ya kukipa uzito au kukitilia mweka kile kisemwacho. Aidha, Cruse (1986) anafanua kwamba sitiari humshawishi msikilizaji (au msomaji) kukitazama kitu, hali au jambo lolote katika sura ya kushabihiana na kitu kingine, kwa kutumia sifa fulani fulani za kitu, hali au jambo la awali kukipambanua kitu, hali au jambo jingine. Kwa mfano, “*Mwameja alikuwa nyani enzi alizokuwa akisimama katika goli la timu ya Simba*”, au “*Ninadhani amezipa akili zake likizo*.” Katika mfano wa kwanza, umahiri wa Mwameja katika kuruka ili kuudaka mpira awapo golini unalinganishwa na urukaji wa nyani awapo kwenye miti; wakati katika mfano wa pili, namna ambavyo mtu anayezungumziwa hutenda mambo pasipo kutumia akili ni kama vile akili zake amezipa mapumziko kwa muda kama ambavyo watumishi hawawi kazini wanapokuwa likizoni.

Fasili hizi za kikamusi hazipambanui vya kutosha dhana ya sitiari kwani hazidokezi hata kidogo sababu za matumizi ya namana hiyo ya lugha na hivyo kuifanya sitiari ionekane kama uholela wa matumizi ya lugha na kutazamwa kama aina fulani ya upotoshaji wa lugha (Cruse, 2011). Cruse anaendelea kufanua namna mbalimbali ambavyo Lakoff na Johnson, (1980), Lakoff, (1987), na wataalamu wengine wamejadili dhana ya sitiari. Katika makala hii, ufafanuzi huo utolewao na wataalamu tunauita mitazamo kuhusu sitiari. Mitazamo hiyo ni kama ifuatavyo.

Sitiari kama Mwingiliano wa Vikoa vya Maana

Kwa mujibu wa Cruse (2011), mtazamo huu ulioanzishwa na mtaalamu aitwaye Haas (1962) ndio unaoitazama sitiari kwa jicho la kiisimu zaidi ikilinganishwa na mitazamo mingine kwa sababu baadhi ya wataalamu (kama Lakoff, 1987) wanaeleza kwamba sitiari si kipengele cha kiisimu moja kwa moja bali ni kipengele kinachohusiana na utambuzi au akili. Kwa mujibu wa mtazamo huu, sitiari hutokea pale ambapo maneno kutoka katika vikoa tofauti hukutana na kuunda kikoa kipya na kusababisha mwingiliano wa vikoa. Kwa mfano, tunaposema “Maisha ni safari” kuna vikoa viwili: kikoa cha maisha na kikoa cha safari. Uelewekaji wa kauli hii hutegemea fahiwa ambazo msikilizaji anazijua kuhusu maisha na kuhusu safari, (kama kukabilia na hatari, vikwazo, uchovu, miiba, njaa, kiu, milima, mabonde, kufika salama, kushindwa kufika, na kadhalika) kisha aunde kikoa kipya cha maana inayokusudiwa (kutokana na safari na maisha). Maana hiyo mpya itakayoundwa ndiyo ijulikanayo kama maana ya kisitiari.

Sitiari kama Ubadala wa Maana

Cruse (2011) anaeleza kwamba mtazamo huu wa sitiari ulijengwa na mwanafalsafa na mwanasayansi Aristotle (aliyeishi kati ya miaka 384 hadi 322 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo) ambaye alizingatia zaidi etimolojia ya neno ‘sitiari’ katika Kigiriki ambako humaanisha “uhawilishaji”. Kwa mujibu wa Cruse (2011), Aristotle aliona kwamba, katika sitiari, kilichokuwa kikihawilishwa ni maana ya kauli moja kwenda katika maana ya kauli nyingine. Hapo ndipo mtazamo wa ‘ubadala wa maana’ katika sitiari ilipoibuka.

Sitiari kama Modeli Analojia

Kwa mujibu wa Cruse (2011), mtazamo huu ulianzishwa na mwanafalsafa wa Kimarekani aitwaye Black. Black (1962), kama alivyonukuliwa na Cruse (2011), anapinga mtazamo wa ‘ubadala wa maana’ na mkabala wa ulinganishaji katika sitiari. Katika modeli hii, Black (1962) anaeleza kwamba utaratibu wa kimuundo na wa kiutendajikazi wa sitiari huhusisha mchomozo wa seti ya vimaanilizi kutoka katika jambo moja kwenda katika jambo jingine. Kwa mfano, mhariri wa gazeti anapoandika kichwa cha habari “CCM kwafuka moshi”, vimaanilizi kadhaa huibuka kikiwamo *kuwapo kwa hali ya hatari ndani ya CCM, hatari itokanayo na migogoro na misugvano ya chini kwa chini*, na kimaanilizi kingine ni kwamba, *ikiwa hali hiyo haitadhibitwa au kupatiwa ufumbuzi wa haraka, basi tutarajie moto kuwaka hivi karibuni (maafa kujitokeza)*.

Sitiari kama Uhusiano kati ya Maana Dhahiri na Maana Fiche

Mtazamo huu uliasisiwa na Sperber na Wilson (1986). Katika mtazamo huu, wataalamu hawa, kama walivyonukuliwa na Cruse (2011), wanatofautisha maana dhahiri na maana fiche katika lugha. Mtazamo huu wa sitiari unajumuisha hoja mbili muhimu. Hoja ya kwanza ni kwamba sitiari haina kitu chochote cha kipekee, bali ni maongezi yasiyo rasmi. Kwa mfano, katika sentensi ‘*wanafunzi walisimama kwenye duara kumzunguka mwalimu*’, hakuna atakayedhani kwamba wanafunzi hao walisimama kwenye duara halisi la kijiometria, bali tunajua kwamba walisimama na kuunda umbo lenye mlandano wa kutosha na umbo la duara.

Sitiari kama Nyenzo Muhimu ya Utambuzi

Cruse (2006 na 2011) anaeleza kwamba nadharia hii iliasisiwa na Lakoff (1987). Lakoff, kama alivyonukuliwa na Cruse (2006, 2011) anasema kwamba sitiari haifanyi kazi ya kupamba lugha tu, bali ni nyezo muhimu ya utambuzi akilini mwa binadamu. Sitiari huhusisha mambo matatu: uwanja chanzi, uwanja lengwa na seti ya uhusiano baina ya nyanja hizo mbili. Mtazamo huu umejikita kwenye hoja kwamba sitiari ni sehemu ya mfumo wa utambuzi au akili za bibadamu.

Sifa za Sitiari

Kutokana na maelezo yaliyotewa na wataalamu mbalimbali kuhusu sitiari (kama Cruse 1986, TUKI 1990, Massamba 2004 na Cruse 2006 na 2011), tunaweza kudondoa sifa zifuatazo za sitiari. Sifa hizi ndizo tutakazozitumia katika tafakuri ya ungonoshaji wa Kiswahili cha mazungumzo iwapo unahusiana na sitiari au la. Kwa muhtasari, sifa hizo za sitiari ni kama zinavyoelezwa hapo chini.

Sifa ya kwanza ni kwamba sitiari hutokea pale ambapo maneno kutoka katika vikoa tofauti vya maana huungana na kuunda kikoa kipya cha maana, hivyo kusababisha mwingiliano wa vikoa. Pili, sitiari inahusiana na ubadala wa maana na hutokea pale ambapo maana ya neno au kauli moja huhawilishwa na kwenda katika maana ya neno au kauli nyingine. Tatu, kimuundo na kiutendaji, sitiari huhusisha kujichomoza kwa seti ya vimaanilizi kutoka katika jambo moja (jambo la msingi) kwenda katika jambo jingine (la ziada). Nne, sitiari ni maana fiche kutoka katika maana dhahiri kulingana na muktadha. Tano, sitiari ni nyenzo muhimu ya utambuzi inayohusisha mambo matatu: uwanja chanzi, uwanja lengwa, na seti ya uhusiano baina ya nyanja hizo mbili. Na sifa ya sita ni kwamba sitiari ni moja ya vyanzo vikuu vya mabadiliko ya maana katika lugha ambapo jambo dhahania hueleweka kupitia jambo dhahiri linalofanana nalo.

Tafakuri ya Upolisemia na Usitiari wa Ungonoshaji

Hakuna kaida ya utumiaji lugha isiyo na dhima maalumu. Ni kwa sababu hiyo basi, tunahitaji kutafakuri iwapo ungonoshaji wa maneno ya Kiswahili katika mazungumzo unahusiana na polisemia au sitiari. Katika kufanya tafakuri hiyo, tunatumia mifano teule sita ya kauli zenye viashiria vya ungonoshaji kutokana na data tulizokusanya. Katika sehemu ifuatayo, vipande sita vya video vyenye viashiria vya ungonoshaji vimefanywa unukuzi na kuwasilishwa na kwa kila moja, tafakuri ya dhima ya ungonoshaji unaojitokeza imefanywa ili kubaini kama ungonoshaji ni polisemia au sitiari. Katika kila unukuzi wa video, maneno yanayovutia au kuchochea ungonoshaji yamekozwa wino. Ifuatayo ni data ya kwanza ambayo ni nukuu ya video mojawapo miongoni mwa video sita zilizoteuliwa.

“...Usipokuwa tayari **kuliwa** kidogo huli. (Vicheko na minong’ono). **Uliwe** kidogo utakula. (Vicheko zaidi). Sasa wewe unataka kula tu bila **kuliwa**? Haiwezekani!” (Vicheko zaidi) ...**Sina maana hiyo!** (Vicheko zaidi na zaidi). Namwona Shehe Khalifa amecheka sana yaani. Sina maana hiyo ya Khalifa. Nina maana hii: tutumie fedha kutangaza, ili sisi tupate zaidi ya hapo...” - Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Bungeni (2006)

Chanzo: Data za uwandani, Novemba 2018

Katika data hii, kuna ungonoshaji unaojitokeza, hasa kwa kukihusisha kitenzi (*ku*)la kilicho katika utendwa yaani (*ku*)liwa. Yaelekea kwamba hapa, ungonoshaji umefanywa na pande zote mbili, yaani mzungumzaji na wasikilizaji. Ilikuwa dhahiri kabisa kwamba, katika muktadha ambamo mazungumzo yalifanyika (Bungeni), Mheshimiwa Rais wa Tanzania wa wakati huo alikuwa anasisitiza haja ya Tanzania kuwa tayari kuyanufaisha mataifa ya nje kwa namna fulani (kuliwa) ndipo nasi kama taifa tuweze kunufaika na misaada ya nchi wahisani (kula). Lakini kurudiwarudiwa kwa maneno *kula* na *kuliwa* ni kiashiria kwamba mzungumzaji alikusudia kukengeusha maana na kuhakikisha kwamba wasikilizaji wanaibua maana ngonoshi katika kile kisemwacho. Wasikilizaji nao walingonosha kilichosemwa kupitia vicheko vyao sanjari na vile vya mzungumzaji. Tunasema hivyo kwani maana msingi ya kauli hiyo ambayo ni: *kukubali kuwanufaisha wahisani ili nasi kama taifa tunufaike* haichekeshi hata iwafanye hadhira wacheke.

Tukitafakuri ungonoshaji unaojitokeza hapa tunabaini kwamba kuna upolisemia na sitiari ndani yake. Upolisemia unaashiriwa pale mzungumzaji anapoibatilisha maana moja kwa kusema “sina maana hiyo”. Maana inayobatilishwa hapa ni ‘maana ngonoshi’ yaani *usipokubali KUFANYWA mapenzi kidogo na mtu unayemwomba msaada huwezi kusaidiwa* (ambayo yeye mwenyewe alifanya jitihada za kujenga akilini mwa hadhira yake kwa kuradidi asemacho hadi alipohakikisha kwamba imetafsirika kingono). Kauli “sina maana hiyo” inaashiria dhima ya kipolisemia ya ungonoshaji kwa sababu, kama tulivyoona hapo juu, polisemia ni chanzo kimojawapo cha utata wa maana katika mawasiliano. Hivyo, kwa kusema tu “sina maana hiyo” tayari mzungumzaji anaonesha kwamba alichokisema kina utata na kinaweza kuwa na maana au tafsiri zaidi ya moja. Ndiyo kusema kwamba kitenzi *kula* (na utendwa wake *kuliwa*) kina dalili za upolisemia na wawasiliani wanaweza kuibua angalau tafsiri hizi: **(ku)la 1** *tia chakula kinywani*; **2** *tia uume ukeni au kwenye utupu wa nyuma wa mwanamume au mwanamke, yaani ngono kinyume cha maumbile*.

Kwa upande mwingine, ungonoshaji unaojitokeza katika data hiyo namba 1 hapo juu unahusiana na sitiari pia, hasa tukizingatia sifa za sitiari zilizodokezwa. Kwa mfano, sifa mojawapo ya sitiari ni kujichomoza kwa vimaanilizi kutoka katika jambo la msingi kwenda katika jambo la ziada. Hili limejitokeza kwa mzungumzaji na wasikilizaji kuhama kutoka kwenye maana msingi yaani, *kukubali kuwanufaisha wahisani ili nasi kama taifa tunufaike*, kwenda katika maana ya ziada yaani, *kukubali KUFANYWA mapenzi na mtu kwanza ndipo baadaye mtu huyo akubali kukusaidia*.

Nyongeza ya hayo ni kwamba, kwa mujibu wa Leech (1981), vimaanilizi vya mazungumzo vina sifa ya kuweza kubatilishwa. Hili limejitokeza pale ambapo mzungumzaji alibatilisha maana ngonoshi ambayo ni *usipokubali KUFANYWA mapenzi kidogo na mtu unayemwomba msaada huwezi kusaidiwa* kwa kusema “sina maana hiyo”. Huu ni uthibitisho kwamba ungonoshaji ni sitiari. Sifa nyingine ya sitiari ni kwamba ina maana fiche kutoka katika maana dhahiri kulingana na muktadha ambapo kiwango cha usitiari kinachoweza kuonekana kuwamo katika kauli fulani hutofautiana kati ya

mtu mmoja na mwingine kutegemea kiwango cha kufanana akionacho mtu huyo. Kwa kuwa maana ngonoshi inayojitokeza hapa si dhahiri ni fiche, basi ungonoshaji ni sitiari. Hebu sasa tuangalie data namba 2 ambayo ni nukuu ya video ya pili miongoni mwa zilizoteuliwa.

“...Huwezi kusema serikali ya CCM haijafanya kitu! Imefanya mambo makubwa. Lakini sasa tatizo la maendeleo, yanahi... **shauku inakuwa kubwa, kadri unavyopanua, ndivyo watu wanavyotamani** au siyo...” (Vicheko). Kwa hiyo sasa mtu... mwenzako ana umeme, wewe huna umeme... (Mzungumzaji ananyamaza kwa muda) Ee, ndiyo! Mheshimiwa Spika nasema hivi... Kadri unavyo... kadri...” (Naye anacheka pia) - Profesa Anna Tibaijuka, Bungeni (2016)

Chanzo: Data za uwandani, Novemba 2018

Data hii namba 2 ina viashiria vya ungonoshaji, hasa kwa kuyahusisha maneno yote yaliyokozwa wino yaani *shauku inakuwa kubwa, kadri unavyopanua, ndivyo watu wanavyotamani*. Kama ilivyo katika data namba 1, hadhira katika data hii inaelewa vizuri kabisa maana msingi inayolengwa na mzungumzaji (ambaye haelekei kudhamiria kungonosha anachokisema hata kidogo). Alichokuwa anaongelea ni ugumu wa kuwaletea wananchi maendeleo kwa kusambaza huduma za jamii kwa sababu watu wote wanahitaji maendeleo. Wana shauku kubwa ya kuletewa maendeleo na serikali yao na inafikia hatua baadhi wanaona kama serikali haiwajali hivi (jambo ambalo si sahihi). Kwa mfano, ukimaliza kupeleka umeme katika kijiji kimoja, kijiji kingine pia kinatahitaji umeme. Ukisambaza maji katika kata moja, kata nyingine inayahitaji pia na kadhalika. Lakini kadiri mzungumzaji alivyoendelea kuzungumza, hadhira ilianza kunong’ona, kucheka, na hata kupiga makofi na kushangilia. Hivyo, shangwe ya hadhira ilimfanya mzungumzaji naye ang’amue kwamba alichokisema kimengonoshwa kwa makusudi tu. Hapo mzungumzaji alicheka huku akijihisi kama amekosea hivi; akataka kuliondoa neno “panua” lakini akakosa neno mbadala.

Tukitafakari ungonoshaji unaojitokeza katika data hii hii namba 2 tunaona unafumbata sitiari zaidi kuliko upolisemia, hasa kwa kuzingatia sifa mojawapo ya sitiari iliyodokezwa katika kipengele kihusucho sitiari hapo juu. Sifa hiyo inasema kwamba *sitiari si pambo la lugha tu bali ni nyenzo muhimu ya utambuzi inayohusisha mambo matatu: uwanja chanzi, uwanja lengwa, na seti ya uhusiano baina ya nyanja hizo mbili*. Tutafafanua jinsi sifa hii inavyojitokeza katika data namba 2 na kutufanya tuihusishe zaidi na sitiari kuliko upolisemia kwa kutumia kifungu cha maneno kilichokozwa wino katika data yaani *...shauku inakuwa kubwa, kadri unavyopanua, ndivyo watu wanavyotamani...* Hebu sasa tuone uwanja chanzi, uwanja lengwa na seti ya uhusiano.

a Uwanja chanzi (maana msingi)

Shauku (hamu kubwa ya kutaka kufanya jambo fulani)

Panua (kitendo cha kuongeza upana au nafasi ya kitu au eneo)

Tamani (kitendo cha kuwa na hamu au haja ya kupata kitu)

b Uwanja lengwa (maana ngonoshi)

Shauku (hamu ya kufanya mapenzi yaani nyege)

Panua (kitendo cha kutawanya miguu ili uke uonekane vizuri au kuongeza upana wa uke)

Tamani (kitendo cha kuwa na hamu au haja ya kufanya mapenzi)

c Seti ya uhusiano (kati ya “a” na “b”)

Neno *shauku* katika uwanja chanzi lina maana ya ‘hamu’ ambapo kuna aina mbalimbali za hamu kama vile hamu ya chakula (yaani njaa), hamu ya kinywaji (yaani kiu) na hamu ya ngono (yaani nyege). Neno hilo hilo *shauku* katika uwanja lengwa limetafsiriwa kama aina mahususi ya hamu, ‘hamu ya ngono’ (yaani nyege). Hivyo ndivyo *shauku* katika uwanja “a” linavyohusiana na maana ngonoshi ambayo neno hilo limebebehsa katika uwanja “b”.

Neno *panua* katika uwanja chanzi lina maana ya ‘ongeza upana.’ Upana huo unaweza kuwa wa kitu au eneo. Katika uwanja lengwa neno hilo lina maana ya ‘tawanya miguu au ongeza upana

wa uke wakati wa kufanya mapenzi.” Uhusiano uliopo kati ya uwanja “a” na uwanja “b” kuhusu neno *panua* ni kwamba, katika kila upande linahusishwa na kuongeza upana. Wakati katika “a”, neno hilo limelenga maendeleo, katika “b”, limelenga ngono.

Neno *tamani* katika uwanja chanzi lina maana ya ‘hisi au kuwa na hamu au haja ya kupata maendeleo’. Katika uwanja lengwa neno hilo limehusishwa na maana ya ‘hisi au kuwa na hamu au haja ya kufanya mapenzi.’ Hivyo, kuna uhusiano baina ya nyanja hizi mbili “a” na “b” kuhusiana na neno *tamani* kwa vile kote msingi wa maana yake ni ‘kitendo cha kuwa na hamu au haja ya kupata au kufanya jambo fulani.’ Tofauti ni kwamba katika “a” kuna *kutamani maendeleo* wakati katika “b” kuna *kutamani tendo la ngono*. Hebu tuangalie data namba tatu ambayo ni nukuu ya video ya tatu miongoni mwa video tano zilizoteuliwa.

“...Uko katikati ya Dar es Salaam; ambayo ni makao makuu ya kibiashara, na Dodoma; ambayo ni makao makuu ya nchi. **Kulala katikati kuna faida yake...** (Vicheko). ...Kwa hiyo mtafaidi ya Dar es Salaam; mtafaidi ya Dodoma. **Katikati ni pazuri...** (Vicheko zaidi). **...Siyo hiyo katikati mnayoichekelea nyinyi...** (Shangwe). Ninasema katikati ya... Mo.ro.go.ro! Watani wangu nyinyi mambo yenu bwana...” Dkt. Johh Pombe Magufuli, Morogoro (2018)

Chanzo: Data za uwandani, Novemba 2018

Katika data hii namba 3, kuna ungonoshaji unaojitokeza, hasa katika maneno yaliyokozwa wino hususani neno *katikati*. Yaelekea kwamba hapa, ungonoshaji umefanywa na pande zote mbili, yaani mzungumzaji na wasikilizaji. Ingawa mzungumzaji anadai kwamba kwa kutumia neno hilo *katikati* anaurejelea mji wa Morogoro ambao upo katikati ya Dar es Salaam na Dodoma, (na kwa kweli hata kimuktadha hiyo ndiyo iliyokuwa maana msingi), kurudiwarudiwa kwa neno hilo *katikati* kulikofanywa na mzungumzaji ni kiashiria kwamba mzungumzaji alikusudia kukengeusha maana na kuhakikisha kwamba wasikilizaji wanaibua maana ngonoshi katika kile kisemwacho. Wasikilizaji nao walingonosha kilichosemwa kwa kucheka sanjari na mzungumzaji na kushangilia. Tunasema hivyo kwa sababu, nje ya ungonoshaji, hatuoni jambo lolote linalochekesha katika ujumbe unaotolewa hapo na mzungumzaji hata liwafanye hadhira kucheka na kuwa na shangwe.

Katika ungonoshaji unaojitokeza hapa kuna upolisemia na sitiari ndani yake. Upolisemia unajitokeza pale mzungumzaji anapoibatilisha maana moja kwa kusema “siyo katikati hiyo mnayoichekelea nyinyi”. Maana inayobatiliwa hapa ni maana ngonoshi: *katikati ya miguu yaani sehemu za siri*, (maana ambayo yeye mwenyewe alifanya jitihada za kuijenga akilini mwa hadhira yake kwa kulirudia neno *katikati* mpaka alipohakikisha kuwa limetafsirika kingono). Kauli “siyo katikati hiyo mnayoichekelea nyinyi” inaashiria upolisemia wa ungonoshaji kwa vile, kwa kusema hivyo maana yake kuna *katikati* nyingi (yaani maana au tafsiri mbalimbali za neno hilo katikati), hivyo kuibua utata wa maana ya kilichosemwa kwa kuchanua maana zaidi ya moja. Kama tulivyoona hapo juu, polisemia ni chanzo kimojawapo cha utata wa maana katika mawasiliano. Kwa mantiki hiyo, neno *katikati* ambalo limengonoshwa lina upolisemia ambapo wawasiliani wanaweza kulitafsiri kama: **katikati 1 sehemu ya kati ya kitu au baina ya sehemu moja na nyingine; 2 sehemu za siri hususani za binadamu (ziwazo katikati ya miguu) au utupu.**

Aidha, ungonoshaji unaojitokeza katika data hiyo namba 3 unahusiana pia na sitiari, hasa tukizingatia sifa mojawapo ya sitiari ya kujichomoza kwa vimaanilizi kutoka katika jambo la msingi kwenda katika jambo la ziada. Tumeona mzungumzaji na wasikilizaji wakihama kutoka kwenye maana msingi ya *katikati* (yaani sehemu ya kati ya kitu au baina ya sehemu moja na nyingine), kwenda kwenye maana ya ziada (yaani *sehemu za siri au utupu hususani wa binadamu*, ambao huwa katikati ya miguu yake). Isitoshe, vimaanilizi (ambavyo ni sifa ya kisitiari) vina sifa ya kuweza kubatilishwa. Hili limejitokeza pale ambapo mzungumzaji alibatilisha maana ngonoshi kwa kusema “siyo hiyo katikati mnayoichekelea nyinyi”, jambo linalothibitisha kwamba ungonoshaji ni sitiari. Sifa nyingine ya sitiari ni kwamba ina maana fiche kutoka katika maana dhahiri kimuktadha ambapo kiwango cha usitiari kinachoweza kuonekana katika kauli fulani hutofautiana kati ya mtu mmoja na

mwingine kutegemea kiwango cha kufanana anachokiona mtu. Ifautayo sasa ni data namba 4 ambayo ni nukuu ya video ya nne miongoni mwa tano zilizoteuliwa.

“...Unajua hakuna boshi yeyote anayempenda mfanyakazi wake... Boshi anapenda kazi yako... Aminini usiamini, ukifa au kuugua, mkeo na wanao wakienda kwa boshi wako kumlilia shida wakati haupo, huyo boshi wako **atammega** mkeo pamoja na watoto wako...” – Msanii ‘Dudubaya’ 2018

Chanzo: Data za uwandani, Novemba 2018

Data namba 4 hapo juu ina ungonoshaji wa wazi na wa moja kwa moja unaofanywa na mzungumzaji, hasa kwa kulihusisha neno *atammega* ambalo limekozwa wino. Tunasema kuna ungonoshaji wa moja kwa moja kwa sababu, tofauti na ilivyokuwa katika data namba 2 (ambapo kuna maana msingi mbali na maana ngonoshi na kwamba kule, hadhira ilielewa vizuri kabisa maana msingi iliyolengwa na mzungumzaji ingawa waliamua kugemea zaidi katika maana ngonoshi), katika data namba 4 muktadha hautuwezeshi kung’amua maana nyingine yoyote ya neno *atammega* tofauti na maana ngonoshi. Ndiyo kusema kwamba, hapa, maana ngonoshi, (ambayo katika mifano mingine huonekana kuwa maana ya ziada), ndiyo hiyo hiyo maana msingi. Ni dhahiri kwamba ungonoshaji katika data hii una usitari na wala si upolisemia kwa sababu haielekei kwamba neno *atammega* linaweza kutafsirika katika namna zaidi ya moja kwa muktadha huu. Katika data hii tunaona kuwa, sifa za kikoa cha mlo zimehamishiwa katika ngono. Tutatumia sifa ya sitiari kufafanua sitiari inayojitokeza katika ungonoshaji wa data ya 4.

a Uwanja chanzi (maana msingi)

Mega (vunja au kata kipande cha kitu kinacholiwa kwa kutumia vidole au meno)

b Uwanja lengwa (maana ngonoshi)

Mega (fanya mapenzi na mwanamke huku yeye akibeba dhima ya utendwa pekee)

c Seti ya uhusiano (kati ya “a” na “b”)

Kinachomegwa ni chakula ambapo neno lenyewe lina fahiwa ya *kuchukua kiasi kidogo toka kwenye kingi badala ya kukimaliza chote*. Hivyo ndivyo boshi anavyoweza ‘kuchukua penzi kidogo toka kwa mjane na watoto wa mfanyakazi wake pindi mfanyakazi huyo anapofariki.

Kwa kuwa kinachomegwa ni chakula na mmegaji hulenga kukidhi haja zake mbalimbali kama vile kufurahia ladha tamu ya chakula, kuondoa hamu ya chakula (yaani njaa) na kuimarisha afya ya mwili wake kupitia virutubisho vya chakula anachokimega na kukila, ndivyo hivyo hivyo pia boshi atakavyokidhi haja zake kama vile kufurahia utamu wa kufanya mapenzi, kuondoa hamu yake ya kingono (yaani nyege), na kuimarisha afya yake ya mwili na hasa akili kwa ‘kuwamega’ mjane na watoto wa aliyekuwa mfanyakazi wake.

Mlaji anapotaka au kuamua kukimega chakula, chakula hakina haki wala nguvu ya kupinga kitendo hicho cha kumegwa hata kama anayekimega si yule aliyekitafuta au kukiandaa na hivyo si yule anayepaswa kukimega na/au kukila. Isitoshe, mmegaji anaweza kuamua kukimega kwa namna yoyote atakayo (mfano bila kunawa mikono) na anaweza kukiacha au kukitupa wakati wowote bila ridhaa ya chakula. Hivyo ndivyo ilivyo hata kwa mjane na watoto wa mfanyakazi aliyefariki mbele ya boshi waliyemfuata ili awape msaada. Watapewa masharti wayatimize ndipo wasaidiwe na shida zao zitawafanya ‘wamegwe’ vyovyote vile na wasiwe na nguvu ya kupinga. Tuangalie data ya mwisho ambayo ni nukuu ya video ya mwisho iliyoteuliwa.

“...Mwili mzima wa mwanamke ni uchi, isipokuwa uso na viganja viwili vya mikono. Sasa wanawake wa leo wanavaa vipedo. Na **mzigo** ukishaingizwa kwenye kipedo sheikh, huwatia fadhaa hata wanaoswali swala tano. Unajikuta tu unaharibu swaumu kwa kuangalia **mizigo** ya watu mwezi mtukufu wa Ramadhani. **Mizigo** mingine ukiiona ni kama haina mwenyewe; ina wenyewe hiyo! Na tembea yao wanafanya makusudi...” - Sheikh ‘Kipozeo’ 2014

Chanzo: Data za uwandani, Novemba 2018

Katika data hii namba tano, ungonoshaji unajitokeza tukiangalia jinsi neno *mzigo* ambalo limekozwa wino lilivyotumika. *Mzigo* ni neno la kawaida ambalo kwa mujibu wa TUKI (2014) maana yake ni *kitu kizito kilichobebwa au jambo lenye kutatiza au lililo gumu kukabiliana nalo*. Lakini *mzigo* inayotajwa hapa na mzungumzaji tunaambiwa inaingizwa kwenye ‘kipedo’ (vazi la kike aina ya kaptura laini inayovutika, yenye kubana na aghalabu, huishia chini ya magoti). Kutokana na fasili hiyo ya neno *mzigo*, ni dhahiri kwamba neno hilo hapa limetumika kisitiari likimaanisha *sehemu ya mwili wa mwanamke iliyojaa kama mzigo (ambayo huingizwa kwenye kipedo)*. Bila shaka ni makalio. Hebu sasa tuangalie kwa nini tunasema neno *mzigo* limengonoshwa kisitiari katika data namba 5 kwa kutumia sifa moja ya sitiari iliyodokezwa hapo awali isemayo: “Sitiari si pambo la lugha tu bali ni nyenzo muhimu ya utambuzi inayohusisha mambo matatu: uwanja chanzi, uwanja lengwa, na seti ya uhusiano baina ya nyanja hizo mbili.”

a Uwanja chanzi (maana msingi)

Mzigo (kitu kizito kilichobebwa au jambo lenye kutatiza au lililo gumu kulikabili).

b Uwanja lengwa (maana ngonoshi)

Mzigo (makalio makubwa au mwanamke mnene na/au mwenye makalio makubwa).

c Seti ya uhusiano (kati ya “a” na “b”)

Tumekwishaona kwamba maana msingi mojawapo ya *mzigo* ni kitu kizito kilichobebwa au kinachotakiwa kubebwa. Kutokana na uzito wake, ni dhahiri kwamba mtu, chombo, au kifaa kitakachoubeba *mzigo* huo kitahangaika katika kuubeba maana nguvu nyingi zitatumika, ili mradi tu shughuli ya kuubeba haitakuwa nyepesi. Huenda mbebaji akatokwa na jasho jingi au pengine akashindwa kabisa hata kuunyanyua *mzigo* huo, sembuse kuubeba. Fahiwa hizi za *mzigo* zimehamishiwa kwa mwanamke mwenye umbo au makalio makubwa katika maana ngonoshi ambapo ugumu wa kuubeba *mzigo* halisi unatarajiwa kuwamo katika kuubeba *mzigo* ngonoshi. Kummudu mwanamke mwenye umbo kubwa au makalio makubwa wakati wa kufanya naye mapenzi linaweza kuwa jambo gumu liwezalo kushindikana mithili ya kubeba *mzigo* halisi.

Maana msingi ya pili ya neno *mzigo* ni jambo lenye kutatiza au lililo gumu kukabiliana nalo. Kama ilivyoelezwa katika maana msingi ya kwanza, utatizaji na ugumu wa kukabiliana na jambo linaloweza kuitwa *mzigo* katika maana msingi ya pili, unahusishwa na ugumu wa kummudu mwanamke mwenye umbo au makalio makubwa wakati wa kufanya au kushiriki naye tendo la ngono. Hapo akili huhitajika kuliko nguvu, kama inavyohitajika tunapokabiliana na jambo gumu.

Jambo la mwisho katika seti ya uhusiano ni furaha na faraja aipatayo mbebaji wa *mzigo* ikitokea ameweza kuumudu uzito wa *mzigo* huo na kuufikisha salama mahali ulikopaswa kupelekwa, au akiweza kulitatua jambo lenye kutatiza au lililo gumu kulikabili. Furaha, faraja, na kujisifu anakoweza kuwa nako mtu huyo ndiko anakoweza kuwa nako mwanamume aliyefanikiwa kufanya ngono vizuri na mwanamke mwenye umbo na/au makalio makubwa. Kwake hayo huwa mafanikio makubwa sana na hujisikia fahari kulisema jambo hilo hadharani.

“...Kama kuna maajabu ya 8 na 9 duniani, basi yapo kanisani... Watu wanaimba wote kwaya kanisani halafu **wanakulana** humo humo. Wanapiga stepu **wanakulana** humo humo! Mwenyekiti **anakula** sauti ya kwanza, Katibu **anakula** sauti ya pili, sijui nani **anakula** sauti ya ngapi, huyu anakula huyu! Hivi tunafanyaje hiyo kazi ya Mungu kama tunaendelea **kulana** namna hiyo?” – Mchungaji Daniel Mgogo, 2019

Chanzo: Data za uwandani, Novemba 2018

Data namba 6 ina ungonoshaji wa moja kwa moja unaofanywa na mzungumzaji, hasa kwa kulihusisha umbo la utendana la kitenzi **kula**, (**kulana**) ambalo limekozwa wino kama lilivyorudiwa mara kadhaa na mzungumzaji. Tunasema kuna ungonoshaji wa moja kwa moja kwa sababu hapa hakuna maana nyingine yoyote ya neno **kulana** tofauti na maana ngonoshi. Ungonoshaji katika data hii unahusiana na sitiari, si polisemia. Tutatumia sifa tatu za sitiari kufafanua sitiari inavyojitokeza katika ungonoshaji wa data hii.

a Uwanja chanzi (maana msingi)

Kulana (kitendo cha huyu kumla yule na yule kumla huyu)

b Uwanja lengwa (maana ngonoshi)

Kulana (kitendo cha kufanya mapenzi au kushiriki ngono)

c Seti ya uhusiano (kati ya “a” na “b”)

Kinacholiwa ni chakula, na chakula ni kitamu na huondoa njaa na kumletea mlaji shibe, nguvu, afya, na aina fulani ya kuridhika. Sasa kwa kuwa wanaoongelewa hapa ni watu, (wala si chakula), na tunaambiwa **wanakulana**, ni dhahiri kwamba neno hilo limetumika kisitiari. Wale wafanyao mapenzi hukidhi haja zao kama vile kufurahia utamu wa kufanya mapenzi, kuondoa hamu zao za kingono na kuimarisha afya zao kimwili na kiakili kwa **“kulana”**.

Hitimisho

Makala hii imetafakari upolisemia na usitiari wa ungonoshaji wa maneno katika Kiswahili cha mazungumzo. Tafakuri hiyo imetuwezesha kubaini kwamba ungonoshaji ni sitiari zaidi kuliko polisemia. Sitiari ndiyo inayodhihirika kirahisi zaidi na hivyo kuonekana kuwa imeshamiri kwa sababu ungonoshaji una viashiria vya mabadiliko ya maana ambapo tunaelezwa na wataalamu kuwa sitiari ni moja ya vyanzo vikuu vya mabadiliko ya maana. Kwa upande mwingine, polisemia ni matokeo ya mabadiliko ya maana baada ya kupitia mchakato wa muda mrefu wa kihistoria na wenye hatua nyingi.

Marejeleo

- Asheli, N. (2011). *Metaphors and Communicative Efficacy in the Headlines of Three Kiswahili Newspapers*. Tasinifu wa Umahiri katika Isimu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- BAKITA, (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.
- BAKIZA, (2010) *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- Campbell, L. (2004). *Historical Linguistics: An Introduction*. Edinburgh: Edinburgh University Press.
- Croft, W. na D. A. Cruse (2004). *Cognitive Linguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Cruse, A. (2006). *A Glossary of Semantics and Pragmatics*. Edinburg: Edinburg Universty Press
- Cruse, A. (2011) *Meaning in Language: An Introduction to Semantics and Pragmatics*. Toleo la 3. Oxford: Oxford University Press.
- Cruse, D. A. (1986). *Lexical Semantics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Elias, S. (2016). Upanuzi wa Maana za Maneno katika Mazungumzo ya Kiswahili. Tasinifu ya Umahiri katika Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar ess Salaam.
- Kibiki, M. J. (2012). Mabadiliko ya Maana katika Vitenzi vya Kiswahili. Tasinifu ya Umahiri katika Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kikwete, J. M. (2006). “Usipokuwa Tayari Kuliwa Kidogo Huli?”. Royal TV katika <https://youtu.be/UdOtv46q4OE>, imesikilizwa 17/10/2016.
- Lakoff, G. na M. Johnson (1980). *Metaphors We Live By*. Chicago: University of Chicago Press.

- Lakoff, G. (1987). *Women, Fire, and Dangerous Things: What Categories Reveal about Mind*. London: The University of Chicago Press Ltd.
- Leech, G. (1981). *Semantics*. Toleo la 2. London: The Penguin Group.
- Makame, H. O. (2015). Maana za Kisitiari Zinavyojitokeza katika Nomino za Kiswahili. Tasinifu ya Umahiri katika Kiswahili (Haijchapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Magufuli, J. P. J. (2018). “Rais Magufuli Akihutubia Morogoro: Katikati ni Pazuri”. Aretas Company katika <https://youtu.be/la6oMYerD4> imetazamwa 10/5/2018.
- Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mgogo, E. (2019). “Wanakwaya Wanakulana Wao kwa Wao Kanisani?”. Mungu ni Mwema Tz katika <https://youtu.be/y23kktFRYsM> imetazamwa 27/5/2019.
- Mwendamseke, F. J. (2016) “Uelekeo wa Maana za Kipolisemia katika Msamiati wa Kiswahili: Mifano kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*”. *Kioo cha Lugha*, 14 (39-49), Dar es Salaam: TUKI.
- Palmer, F.R. (1976) *Semantics: A New Outline*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Reuster-Jahn, U. na R. Kießling (2006) ‘Lugha ya Mtaani’ in Tanzania: The Poetics and Sociology of a Young Urban Style of Speaking; katika *Swabili Forum*, Na. 13, Toleo Maalumu, (1-87). Mainz Germany: Idara ya Anthropolojia na Taaluma za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Johannes.
- Saeed, J. I. (2004). *Semantics*, Toleo la 2. Oxford: Blackwell Publishing Ltd.
- Shaweji H. (2014). “Wanawake na Vipedo -Sheikh Kipozeo”. Mpita Njia katika <https://youtu.be/WBiEpDaziKw> imetazamwa 30/1/2019
- Tibaijuka, A. (2016). “Prof. Tibaijuka: Kadri Unavyopanua Ndivyo Watu Wanavyotamani?”. O Channel katika <https://youtu.be/JNWi8TsRUBg>, imetazamwa 30/11/2017.
- TUKI, (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- TUKI, (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la 3. Nairobi: Oxford University Press.
- Ullmann, S. (1962). *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Blackwell.